




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA



TANGAZO LA ZABUNI

TAREHE 14.05.2023

1. Mwaliko huu wa Zabuni (MZ) unafuatia Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
2. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga fedha kwaajili ya utendaji kazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Halmashauri ya Manispaa ya Songea itatumia sehemu ya fedha hizo kwa ajili ya zabuni ya Huduma ya ulinzi, Huduma ya uzoaji wa taka na Huduma ya ukusanyaji wa ushuru.
3. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea anayo furaha ya kuwaalika zabuni kutoka kwa watu Binafsi, Makampuni, *Ushirika*, *Taasisi au Vikundi* vya watu vilivyosajiliwa *kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa Zabuni zifuatazo:-*
4. ZABUNI YA KUFANYA USAFI, KUKUSANYA TAKA NGUMU KWENYE MAKAZI YA WATU, MAJENGO YA BIASHARA, MASOKO, STENDI ZA MABASI, MITAA NA OFISI MBALIMBALI KUZOA TAKA NA KUKUSANYA ADA ZA TAKA KATIKA KAYA ZOTE KATA ZA MJINI, MAJENGO NA MFALANYAKI KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA Namba ya Zabuni: NA.LGA/103/2023/2024/NCS/46 LOT 1
5. ZABUNI YA KUFANYA USAFI, KUKUSANYA TAKA NGUMU KWENYE MAKAZI YA WATU, MAJENGO YA BIASHARA, MASOKO, STENDI ZA MABASI, MITAA NA OFISI MBALIMBALI KUZOA TAKA NA KUKUSANYA ADA ZA TAKA KATIKA KAYA ZOTE KATA ZA MISUFINI, MATARAWA, BOMBAMBILI KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA Namba ya Zabuni: NA.LGA/103/2023/2024/NCS/46 LOT 2

6. ZABUNI YA HUDUMA YA ULINZI KATIKA OFISI KUU YA MANISPAA, DEPOT, KITUO CHA AFYA MJIMWEMA, KITUO CHA AFYA RUVUMA NA STENDI YA TANGA.
Namba ya zabuni LGA/103/2023/2024/NCB/45
7. Nyaraka za zabuni hizi zinapatikana katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Songea Kitengo cha Manunuzi kuanzia tarehe 14.05.2023 mpaka tarehe 28.05.2023 Siku za kazi saa 07:30 Asubuhi hadi saa 15:30 Alasiri.
8. Zabuni hizi zitapatikana kwa gharama ya Tsh.50,000 kwa zabuni moja. Malipo yote yatafanyika kupitia Control Number utakayo pewa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Manispaa ya Songea Kitengo cha Mapato na Mwombaji anapaswa kuwasilisha risiti ya malipo ya zabuni husika wakati wa kuchukua nyaraka ya zabuni.
9. Maelezo kwa kina yanapatikana katika nyaraka ya zabuni husika au fika katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Songea Kitengo cha Manunuzi kuanzia tarehe ya Tangazo hili mpaka mwisho wa Tangazo siku za kazi kuanzia saa 07:30 Asubuhi hadi saa 15:30 Alasiri
10. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA S.L.P 14 KWA KATIBU WA BODI YA ZABUNI (KITENGO CHA MANUNUZI) kabla au ifikapo Tarehe 28.05.2023 saa 10:30 Asubuhi.
11. Mara tu baada ya muda wa mwisho kufika zabuni zote zitafunguliwa mbele ya wazabuni, wawakilishi wa wazabuni na Wananchi wote watakaopenda kushiriki katika zoezi la Ufunguzi.
12. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa nje ya muda au kwa njia isiyoruhusiwa hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yeyote
13. Tathimini ya zabuni itafanywa kulingana miongozo na sheria za ununuzi wa umma.
14. Nyote mnakaribishwa.



Dr, Frederick D. Sagamiko
Mkurugenzi wa Manispaa

Halmashauri ya Manispaa ya Songea